**NATIONAL NETWORK OF TANZANIAN WOMEN WITH HIV/AIDS**

**(NETWO+)**

**P.O. Box 71489, DAR ES SALAAM TANZANIA,**
**E-MAIL: netwo2002@yahoo.com**
**TEL: 255-744-360 075, FAX: 255-22-2110449**

**RISALA YA MWENYEKITI WA MTANDAO WA TAIFA WA WANAWAKE WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI NA UKIMWI (NETWO+) - MPENDWA ABINERY CHIHIMBA KATIKA TUKIO LA KUWASHA MISHUMAA ILI KUWAKUMBUKA WANAWAKE WALIOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI NA KISHA WAKAFARIKI KWA UKIMWI, IKIWA NI SEHEMU YA MAADHIMISHO YA MIAKA 10 YA AZIMIO LA BEIJING NA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 2005:**

**UKUMBI: KARIMJEE.**
**MGENI RASMI: WAZIRI MKUU MH. FREDRICK T. SUMAYE (Mbunge)**

Mhe. Frederick.T. Sumaye Waziri mkuu wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Dr, Asha Rose Migiro Waziri wa wizara ya Maendeleo ya jamii, jinsia na watoto

Waheshimiwa mawaziri na naibu waziri

Mhe Muwakilishi wa mkuu wa mkoa wa Dar es salaam.

Waheshimiwa wabunge.

Waheshimiwa mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa na kitaifa.

Waheshimiwa viongozi wa dini mliopo hapa.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana .

Mheshimiwa waziri mkuu kabla ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushuru kwa kukubali kuwa mgeni Rasmi katika shughuli hii ya kuwasha mishumaa ili kuwakumbuka wanawake wote walioishi na Virusi vya UKIMWI,na kisha wakafariki kwa UKIMWI.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naomba uniruhusu nitoe shukrani kwako kwa niaba ya wanachama wa NETWO plus, na kwa niaba ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwa kukubali kwako kuhudhuria hafla hii.

Mheshimiwa tunaelewa majukumu yako ni mengi kwenye ujenzi wa taifa, lakini umechukua muda wako kujumuika nasi, hatua hiyo inaonyesha upendo, huruma na heshima uliokuwa nayo juu yetu sisi tunaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mgeni rasmi,NETWO ni mtandao wa Taifa wa wanawake na wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI,Tanzania. Mtando huu ulianzishwa mwaka 2002 kwa ushirikiano wa wanawake wanaoishi na virusi vya UKIMWI kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania walipokuwa wakihudhuria mafunzo yaliyoandaliwa na Chama cha Wanawake wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI Tanzania kwa ushirikiano na UNICEF Tanzania. Mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo wanawake wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, yaliendeshwa na Mabalozi wa mtandao wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI barani Africa (NAP+ Ambassadors of Hope) ambao nao pia wanaishi na virusi vya UKIMWI. NAP+ ni wahimili wakubwa wa mpango huo wa Mabalozi wa matumaini barani Afrika.

Kazi kubwa ya mabalozi wa matumaini ni kutoa mafunzo kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI barani Afrika katika eneo la namna ya kuwa wazi (going public) kuhusu hali yao ya kuishi na VVU. Pia kuwawezesha kuunda vikundi ili waweze kuhesabika na kusaidiwa hasa na serikali zao pindi ipatikanapo misaada. Kazi nyingine ni kuielezea hali halisi ya kuishi na VVU na UKIMWI katika uso wa dunia.

Mhe. Waziri Mkuu, Madhumuni ya NETWO+ ni kutoa mafunzo kwa wanawake wanaoishi na wa Virusi vya UKIMWI, kupeana habari za mabadiliko mbalimbali yanayotokea duniani kote kuhusiana na janga zima la UKIMWI.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, leo tumejumuika hapa kwenye shughuli hii ya kuwasha mishumaa kwa sababu zifuatazo:

1. Kuwakumbuka wanawake ambao walikuwa ni ndugu, jamaa, marafiki na wapendwa wetu, walioishi na VVU na kisha wakafariki kwa UKIMWI.
2. Kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kutulea ili tuweze kuhimili misukosuko inayotokana na UKIMWI.
3. Kuonyesha ishara ya upendo baina yetu.
4. Mwangaza wa mishumaa uwe dalili ya matumaini kuwa tunaweza kumshinda adui UKIMWI.

5. Kujenga mshikamano wa taifa kwenye vita dhidi ya UKIMWI.
6. Kutoa kiapo kuwa tutailinda na kuitekeleza sera ya taifa ya kudhibiti UKIMWI.
7. Kufurahia maisha.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nasema kufurahia maisha kwa sababu wakati wa majonzi umekwisha, sasa tunataka kusonga mbele kwa kasi mpya yenye mwelekeo mpya.

Hatukatai kuwa UKIMWI umelirudisha na unaendelea kulirudisha taifa letu nyuma lakini wakati wa malalamishi umepitwa, sasa tunalihitaji mwelekeo mwingine - tunasema "tunataka kuishi kwa matumaini", kuishi kwa matumaini kunamaanisha tuondokane na kukata tamaa, kugombana wenyewe kwa wenyewe na kulaumiana, badala yake, tujumuishe nguvu zetu zote kumshinda huyu adui.

Mhe. Waziri Mkuu, mambo mengi yamesemwa na mengi yanaendelea kusemwa kuwa sisi tunaoishi na virusi vya UKIMWI hatuna umoja wala upendo baina yetu. Kwa kiasi kikubwa, hiyo ni sahihi lakini naomba jamii ielewe kuwa sisi tunaoishi na virusi vya UKIMWI tunakabiliana sio tu na ugonjwa wenyewe unaoleta homa, maumivu na magonjwa tegemezi mengineyo. Sio tu tunaishi na hofu kuwa kinga zetu zinaweza kupungua hadi kufikia umauti wetu, lakini pia tunaishi kwenye jamii ambayo baadhi yao wanakataa kuwa na huruma kwa watu walioambukizwa virusi vya UKIMWI.

Hebu fikiria Mheshimiwa, mizigo tunayobeba - kunyooshewa vidole, unyanyapaa, ubaguzi, kuachishwa ajira inapogundulika tumeambukizwa virusi vya UKIMWI.

Sisi tumekubali jukumu hilo na tunaamini taifa limepiga hatua kubwa kwa vile tunaoishi na virusi vya UKIMWI tumevunja UKIMYA, na tumejitokeza hadharani kwa uwazi.

Kuwa wazi ni muhimu kwa sababu mbili - kupunguza kasi ya maambukizi, na kupata msaada kwa watu na familia zilizoathirika na UKIMWI.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni "UKIMWI una sura ya mwanamke", mwanamke huyo ni sisi wanachama wa NETWO plus, mwanamke huyo ni yule mama aliopo nyumbani anaishi kwa uaminifu, kumbe mumewe ameleta UKIMWI ndani ya familia, mwanamke huyo ni yule msichana anaetafuta riziki ya halali ofisini na bosi anamwambia "lazima ufanye ngono na mimi, au utakosa ajira", mwanamke huyo ni bibi alieachiwa wajukuu kulea ambao wazazi wao

wamefariki kutokana na UKIMWI, mwanamke huyo ni yule mjane anaedhulumiwa mirathi yake na ya watoto wake na ndugu wa marehemu mumewe aliefariki kwa UKIMWI, mwanamke huyo ni yule muuguzi anaetunza mgonjwa wa UKIMWI bila hata ya kupatiwa mafunzo au vitendea kazi, mwanamke huyo ni yule binti anaekeketwa, mwanamke huyo ni yule mama anaeletewa mitala na hathubutu kulalamika, mwanamke huyo ni yule binti aliebakwa, mwanamke ni yule anaekosa dawa za kupambana na virusi vya UKIMWI (ARV) kwa kuambiwa mwanaume ndiyo mtunzaji wa familia, acha yeye mwanaume apewe dawa za ARV kwanza. Lakini naomba nikumbushe kwamba "mwanamke ni nguzo ya maendeleo, Mpe nafasi."

Sasa Mheshimiwa hebu angalia mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI anapokuwa mwanamke. Huo mzigo tunaoubeba sisi wanawake tunaoishi na virusi vya UKIMWI unakuwa maradufu.

Tunabeba adha na misikusuko ya kuumwa, tunaitwa wazinzi, wajaa dhambi, tunaambiwa tumeua waume zetu kwa kupeleka UKIMWI kwenye familia, tunabaki na ulezi wa watoto yatima, tunakosa haki zetu kwenye mirathi.

Kwa ufupi Mheshimiwa, unapokuwa mwanamke, hadhi yako kwenye jamii inakuwa duni. Unapokuwa mwanamke anaeishi na virusi vya UKIMWI, hadhi inazidi kuporomoka, hata kufikia wengine kuchanganyikiwa. Sababu hizi zimetulazimisha Kuunda Mtandao wa NETWO plus.

Ilituchukua muda kabla hatujajisajili kwa vile hatukua na pesa za gharama ya kusajili lakini hatimaye baada ya kuchangishana wenyewe tuliweza kupata hati ya usajili, Asante Mwenyezi Mungu. Tatizo kubwa tulilobakiwa nalo ni ukosefu wa vifaa vya ofisi na ofisi ya kudumu, kwani tunatumia kwa muda ofisi ya Vijana Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI iliyopo Magomeni karibu na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, pia ukosefu wa rasilimali ya kuendeleza mipango tuliyojiwekea ikiwemo, mafunzo mbalimbali kama ya ufahamu wa matibabu (treatment literacy), uongozi (katika mtizamo kwamba vikundi vyetu tumeunda kwa sababu ya kuwa na VVU na sio kwa sifa ya ujuzi).

**DIRA** yetu ni kuhakikisha kuwa wanawake wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI tunapata heshima, utu na haki zetu kama tunavyostahili.

Mara kadha Mheshimiwa umekuwa ukisema "Taifa halitaweza kushinda vita dhidi ya UKIMWI bila ya mchango wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI." Tamko lako Mheshimiwa limeleta faraja kwetu kuwa umuhimu wetu kwenye jamii unatambuliwa.

Mhe. Waziri Mkuu, tunayo mengi ya kuongea na jamii pamoja nawe, hasa ukizingatia kuwa katika historia ya zaidi ya miaka 21 toka VVU na UKIMWI kuingia Tanzania, leo ni mara ya kwanza kwa sisi wanawake tunaoishi na VVU na UKIMWI kwa pamoja kukutana nawe na sisi kukutana pamoja na kujadili mambo muhimu yanayotuhusu kama tulivyofanya leo kuanzia asubuhi hadi jioni katika kongamano la siku moja. Hapa napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Wizara ya Maendeleo ya jamii, Jinsia na watoto kwa kutushirikisha na kutusaidia sisi wanawake tunaoishi na VVU na UKIMWI kutoka mikoa mbalimbali hadi tukaweza kukutana katika maadhimisho haya.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**